BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 30 Septemba, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bajeti kwa mwaka 2023/2024.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bajeti kwa mwaka 2023/2024.

III. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Ikulu:

32. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

Serikali huwatumia wataalamu wa nje ya Zanzibar katika kutengeneza Mifumo ya TEHAMA hapa Zanzibar.

Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuhakikisha wataalamu hao wanapatikana hapa nchini.

## Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

277. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Likizo ya mwaka ni haki ya kila mtumishi wa umma kwa mujibu wa sheria na kanuni za utumishi wa umma wa Zanzibar. Hata hivyo, kuna malalamiko kwamba baadhi ya taasisi zimekuwa zikikiuka makusudi sheria na kanuni hizi ya yakuwapatia wafanyakazi haki yao ya likizo ya mwaka, ikiwa ni pamoja na malimbikizo ya likizo hizo mpaka miaka miwili hadi mitatu.

(a) Je, Serikali yetu inalitambua vipi tatizo la baadhi ya taasisi kutowapa wafanyakazi haki yao ya likizo ya mwaka kwa muda mrefu, na ni hatua gani inachukua kwa waajiri husika.

(b) Je, vipi Serikali inafuata taratibu za kisheria na kikanuni za kupokea malalamiko ya watumishi wa umma ambao hawakupata likizo kwa muda mrefu na ni namna gani inayashughulikia malalamiko haya.

(c) Kwa kuwa Mtumishi wa Umma anapopokea likizo anatakiwa kupata posho, je, posho hizi hupelekwa wapi kwa wafanyakazi ambao hawakupata likizo ya mwaka.

## Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

19. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Ni kwa kiasi gani mikopo chechefu inapunguwa mwaka hadi mwaka katika Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

20. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kumekuwa na mabadiliko ya matumizi ya mifumo ya teknolojia katika mifumo mbali mbali ya fedha ili kuzuia mianya ya upotevu wa fedha.

Je, mabadiliko haya yanayofanywa mara kwa mara katika mifumo hii, ni kwa kiasi gani yameweza kugundua matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

124. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kwa kiasi gani Serikali imefanikiwa kuondoa tatizo la kukosa mikataba kwa waajiriwa hususani wanaofanya kazi katika sekta binafsi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

132. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kiasi gani walimu waliobobea katika lugha ya Kiswahili kutoka Zanzibar wananufaika na fursa za kufundisha lugha ya Kiswahili katika Balozi zetu 19 zilizofungua vituo vya kitamaduni (cultural centres) kupitia mataifa hayo.

133. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ni fursa zipi ambazo wananchi wa Zanzibar wananufaika nazo kutokana na kuwepo kwa Makao Makuu ya Kiswahili, Afrika Mashariki.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

95. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Wanaume wengi wamejikuta wakipata hatia ya kuhukumiwa jela kutokana na kesi nyingi za kusingiziwa kubaka.

(a) Je, Wizara yako inatumia utaratibu upi wa kuhakikisha kwamba wanapata ushahidi unaojitosheleza katika kesi hizo.

(b) Je, ni ipi hatua stahiki anayopatiwa mtuhumiwa baada ya kutolewa hukumu na kubainika kuwa hakutenda kosa.

**Wizara ya  Maji, Nishati na Madini:**

258. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kijiji cha Mavuika, Kinyuji, Mtangamle na Jirambe ni vijiji vinavyopatikana katika jimbo la Mtambwe, shehia ya Mtambwe Kusini. Vijiji hivi kwa muda mrefu vimekuwa vikiiomba Serikali kuwafikishia huduma za kijamii ikiwemo huduma ya umeme ili waweze kujikwamua kimaisha kwa kukuza shughuli za maendeleo.

(a) Je, Serikali inafahamu kilio cha wananchi hawa na ni lini wananchi hawa wategemee kupata huduma hii ya msingi.

(b) Je, kwa takwimu ni vijiji vingapi vipya katika kila Wilaya vimeungwa umeme katika mwaka wa fedha 2023/2024.

(c) Ni ipi mipango ya Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) katika kufanikisha azma ya Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi ya kufikisha umeme katika kila kijiji nchini.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

29. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni upi mkakati wa Serikali wa kuwawezesha wakandarasi  wa ndani ili waweze kufikia soko la ushindani  hasa kwa miradi mikubwa.

80. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tathmini iko vipi juu ya kupatiwa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa mradi wa kimkakati wa ‘flyover’ kutoka eneo la Kwamabata hadi Amani Tigo.

**Wizara ya Afya:**

99. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Ni juhudi zipi zilizofanywa kupitia Taasisi ya Utafiti wa Afya kuhusiana na ubora wa maendeleo ya lishe kwa watoto walio chini ya umri wa miaka minne.

111. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

     Lishe na afya bora ndio msingi wa taifa bora na imara, pia tafiti zinaonesha kwamba uzalishaji wa mboga mboga kwa asilimia 70 unatumia mbolea za kemikali ambazo zina madhara makubwa kwa afya ya mlaji.

     Kwa kiasi gani kampeni ya lishe bora ya matumizi ya mboga mboga inaweza kufanikiwa.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

82. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    Mahamam ni moja kati ya alama za historia kubwa ya ukomavu wa uchumi na ustaarabu wa Zanzibar katika miongo ya karne nyingi zilizopita nyuma.

    (a) Je, tuna mahamam (masauna) mangapi yanayohifadhiwa kwa sasa na kutembelewa na watalii wanaokuja nchini kwetu.

    (b) Ni kwa kiasi gani mahamam haya yanaendelea kuakisi na kuielezea historia ya Zanzibar kwa upekee wake.

    (c) Baadhi ya mahamam yameshavamiwa na makaazi ya wananchi likiwemo lile la kidichi. Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya kulipatia hatimiliki hamam hilo.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

46. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    (a) Tathmini iko vipi juu ya mkakati wa Serikali wa kusomesha madaktari wa wanyama wasiopungua 20 katika kufikia malengo yanayotarajiwa.

    (b) Tathmini iko vipi juu ya malipo sawa ya mishahara kwa madaktari wa wanyama na madaktari wa binaadamu.

105. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Sayansi ya kilimo imeleta mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo.

    (a) Ni kwa kiasi gani kuingia kwa miti mingi ya kupandishia kwa mfumo wa 'budding' kumepelekea kupoteza miti ya asili katika uasili wake.

    (b) Tathmini iko vipi juu ya mtazamo wa wakulima wengi kuacha kupanda miti ya asili katika uasili wake na badala yake kushajiika kupanda miti ya aina ya kisasa na ya kupandishia.

## IV. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bajeti kwa mwaka 2023/2024.

.

**Zanzibar,**
**30 Septemba, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**